JE, UNADHANI UNA SURUA?

Cha kufanya ikiwa unadhani una surua

Surua kawaida huanza na homa, kikohozi, pua inayotokwa na kamasi, na macho mekundu, kisha hufuatiwa na vipele. Ikiwa mtu katika familia yako ana dalili za surua:

Waweke mbali na wanafamilia ambao hawajaugua.

Kila mtu ndani ya nyumba anatakiwa kubaki nyumbani ili wasiaambukize majirani au watu wengine nje ya nyumba.

Piga simu kwa daktari au hospitali mara moja kuwaarifu kwamba kuna mtu nyumbani kwenu ana surua.

Wakati wa kwenda chumba cha dharura

Ikiwa mgonjwa anazidi kuwa na hali mbaya haraka au ana mojawapo ya dalili zilizo hapa chini, mpeleke haraka kitengo cha dharura hospitalini.

USISUBIRI.

Shida ya kupumua
(au kupumua haraka kuliko kawaida)

Maumivu wakati wa kupumua au kukohoa

Upungufu wa maji mwilini
(pua na mdomo kukauka, kukojoa kidogo, kulia bila kutoa machozi)

Homa au maumivu ya kichwa yasiyokoma

Kuchanganyikiwa, kupoteza ufahamu, au udhaifu mkubwa

Rangi ya buluu kuzunguka mdomo, uchovu mwingi, au kushindwa kunyonya
(kwa watoto wadogo)

Mwambie mtu apige simu kabla hujafika. Arifu hospitali kwamba mgonjwa wa surua anakuja.